



Ubia Mkakati wa Zao la Parachichi

Muhtasari

Parachichi (*Persea americana*) ni mti, mrefu unaosemekana asili yake ni Kusini Kati mwa nchi ya Mexico. Tunda la mmea, pia linaitwa parachi (au avocado pear au alligator pear), ni asili ya mmea wa tunda kubwa linalokuwa na mbegu kubwa inayokulikana kama "shimo" au "jiwe". Parachichi kama yalivyo matunda mengi yenye virutubisho ya lishe yana thamani kubwa ya kibiasara na kulimwa sehemu zenyen ukanda wa kitropiki na mediteranea duniani kwote. Kiwango cha hali ya afya ya udongo unaofaa kustawi kwa parachichi ni kati ya pH 6.2 na 6.5. Kituo cha Kimataifa cha Biashara (ITC), Tanzania imeshuhudia uuzaji nje ya nchi ukukua kwa CAGR ya asilimia (35%), kutoka mwaka 2013 mpaka 2017, ikikaribia tani za ujazo elfu 4.4 mwaka 2017 kutoka tani za ujazo elfu 1.4 mwaka 2013.

Nchini Tanzania, uzalishaji wa Parachichi unaanza kufahamika mimongoni mwa jamii huku mashamba mapya yakiendelea kufunguliwa maeneo mbalimbali nchini. Mikoa kama ya Njombe, Iringa, Geita na hata mikoa wa Kagera kumeshuhudiwa ongezeko la maeneo yaliyopandwa na hutoa mavuno makubwa; aina inayopandwa kwa ajili ya soko la nje – Hass na Fuerte. Mikoa mingine ambapo parachichi hulimwa ni Arusha, Morogoro, Kilimanjaro, Mbeya, Songwe and Ruvuma. Parachichi linahitajika sana kwenye soko la dunia kwa sasa na kuweza kuchangia mapato ya fedha za kigeni na mapato kwa Serikali kama litasimami vizuri.

Mbali ya kuongezeka kwa ukubwa wa mauzo ya nje ya nchi, kuna hamu ya Uwekezaji katika kuongeza thamani ya Parachichi. Kongani ya lhemu viko viwanda viwili, mkoani Iringa kipo Zalacado na mkoani Njombe kipo Olivado.

Wadau Muhimu walioko kwenye Ubia wa Parachichi

- Sekta ya Umma
- Sekta Binafsi
- Washirika wa Maendeleo
- Asasi za Wakulima
- Mkulima mmoja mmoja
- Asasi za Kiraia

Mpango wa Kukuza Kilimo kwenye Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT)

Mpango wa SAGCOT ni ubia katika sekta ya umma na binafsi unaolenga kuchoechea Uwekezaji kwenye Kilimo biashara katika ukanda wa kusini mwa Tanzania. Kituo cha SAGCOT kinafanya kazi kama dalali wa ubia na kitovu cha habari kwa wabia wa SAGCOT katika kuwezesha uwekezeshaji kwenye minyororo ya thamani inayoshirikisha jamii na kuzingatia uhifadhi endelevu wa mazingira. Kila mwaka, aina mbalimbali za ubia mkakati zimeibuka ambazo Mpango wa SAGCOT unashiriki kikamilifu kukuza na kuwezesha kutoptana na Matukio makuu na yanayoweza kupanua shughuli hizi.



Nini kinasabisha ubia wa parachichi kuwa ubia mkakati?

Kiushindani, Kenya imekuwa nchi ya 6 kwa uzalishaji mkubwa wa parachichi duniani mwaka 2017, wakati Tanzania imenorodheshwa kuwa nchi ya 20 kwa uzalishaji mkubwa duniani. Thamani ya mauzo imebakia kuwa ni ya chini ukilinganisha na nchi nyininge zinazouza parachichi ambapo Kenya, Tanzania na Afrika Kusini zinazuwa kwa bei ya chini zaidi kwa sababu ya umbali wa masoko ya parachichi na walaji katika masoko hayo kushindwa kutambua thamani ya parachichi zitokazo kwenye nchi hizi tatu.

Tanzania inafaidika na hali nzuri ya hewa inayoifanya kuwa ni nchi inayoongoza kwenye uzalishaji wa parachichi ukanda wa Afrika Mashariki. Endapo jitihada za wauzaji wa nje, wakulima na serikali zitaratibiwa vizuri, kuna fursa muhimu katika kuongeza mauzo ya parachichi duniani.

Kuimarika kwa usalama wa chakula na hali ya maisha katika kaya.

Parachichi inatoa mchango mkubwa sana katika kuboresha lishe na usalama wa chakula katika Ukanda wa SAGCOT na nje ya ukanda kutoptana na kuwa na kiasi kikubwa cha protini na madini kulinganisha na protini ya wanyama. Kiuchumi, tunda lina faida ya kupata soko zuri ndani ya Tanzania na soko la kimataifa na kulifanya kuwa ni chanzo kizuri cha mapato kwa wakulima na fedha za kigeni.

Kutafuta masuluhisho ya kudumu katika mnyororo wa thamani

Ubia wa Parachichi unalenga kukuza biashara binafsi katika usimamizi wa vitalu ili kuongeza idadi ya miche, Uwekezaji katika mbinu za kisasa za Kilimo na huduma za ugani, Uwekezaji kwenye skimu za umwagiliaji, kuongeza uzalishaji wa parachichi aina ya Hass ili kukidhi mahitaji ya soko, uwekezaji kwenye vyumba baridi nya kuhifadhi na kusaka masoko anuui ya nje. Kufuatia mpango wa serikali wa kujenga chumba baridi cha kuhifadhi katika uwanja wa ndege wa Songwe, ndege za kimataifa zinazobeba mizigo hivi punde zitaanza kusafirisha parachichi na mazao mengine ya matunda na mbogamboga moja kwa moja kwenda kwenye masoko ya kimataifa.

Serikali pia ipo kwenye mchakato wa kujenga jingo lijulikanalo kama ukanda wa kijani katika bandari ya Dar-es-Salaam kwa ajili ya kuhifadhi bidhaa/mazao yanayoharika mapema ikiwemo parachichi.

Kuwakutanisha wabia

Ushiriki wa Wadau kupitia Ubia wa Parachichi unalenga kuanzisha jukwaa la mashauriano kwa watendaji wote wa mnyororo wa thamani kushughulikia Changamoto kwa pamoa. Wabia wa SAGCOT wamewekeza ndani ya ukanda katika uzalishaji, nyumba za kufungashia na vyumba baridi. Wadau muhimu katika ubia wa parachichi wakijumuisha Tanzanice, Lima Kwanza, Kuza Africa, GBRI, Kibidula farm, Olivado, na Washirika wa Maendeleo wanaosaida kifedha miradi kama Mboga na Matunda, TAHA, Wakala wa Serikali na Wizara kama vile Southern Highlands Region Secretariat, na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Wizara ya Kilimo, TAMISEMI, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), Kituo Cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Kituo Cha Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI).

Takriban wadau 600 wameshiriki katka Mkutano wa Uwekezaji katika Kilimo cha Matunda na Mbogamboga uliofanyika mwezi Juni 2020 mkoani Mbeya wakiwemo sekta ya umma (mamlaka za serikali kuu na mitaa), mamlaka za usimamizi/udhibiti, washirika wa maendeleo, sekta binafsi (wawekezaji wa nje na ndani ya nchi), asasi zisizo za kiserikali, taasisi za utafiti, wafanyabiashara (wanaouza nje ya nchi), wakulima, na taasisi za kifedha

Ubora wa mazao na manufaa kwa wakulima

Wakulima wadogo ndio wazalishaji wakubwa wa parachichi lakini tija ya uzalishaji wao ni ndogo kulinganisha na Mashamba makubwa yanayomilikiwa na kampuni binafsi, Kampuni binafsi zinazalisha mpaka tani 21/hekta ya matunda katika shamba lenye ukubwa wa eka 100 kulinganisha tani 9/hekta kwa Wakulima wadogo katika shamba lenye ukubwa unaokadirwa kuanzia 1/8 ya eka na eka 2. Kumekuwepo na jitihada kubwa katika upanuzi wa mashamba madogo/kati kwa kuwapatia miche, kuwapa msaada wa Kilimo cha kitaalam, pembejeo na vifaa nya kuvunia.

Kuonyesha Matokeo chanya ya kimazingira.

Wengi wa wazalishaji wadogo wa parachichi wanao uelewa juu ya umuhimu wa matumizi ya maji kwa ufanisi, lakini hawatumii maarifa walijonayo kwenye matumizi ya maji na teknolojia za uvunaji kutokana na gharama kubwa za kufanya hayo. Umwagiliaji ni muhimu kwa mti michanga lakini sio lazima kuwa mti ambaa hautavunwa, sababu msimu wa parachichi wa SAGCOT ni tofauti na kanda nyingine zilizoko maeneo mengne duniani. Kwa hiyo, Wakulima wanayo nafasi ya muda kati ya Machi mpaka Juni na Septemba mpaka Oktoba kuyapeleka maparachichi yao kwenye soko la kimataifa, na kupata bei nzuri kwa sababu kipindi hiki kawaida sio msimu wa biashara kwa wazalishaji wa parachichi kwenye nchi nyingine.

Matokeo Jumuishi na endelevu

Tathmini ya Uharibifu wa Wadudu juu ya athari jumuishi na endelevu kwenye Kilimo cha parachichi imefanya na Wizara ya Kilimo kuhakikisha Viwango nya soko la dunia vinakidhi na kuongeza ubora wa maparachichi ya Tanzania kwenye masoko ya kimataifa kama vile Umoja wa Ulaya, China, India, Afrika Kusini na masoko mengine muhimu. Fursa za ajira katika mnyororo wa thamani wa parachichi ziko wazi kwa mtu ye yeyote bila kujali jinsia yake. Hata hivyo, aina ya kazi zinatofautiana kati ya wanaume na wanawake hata kama wana kiwango kinacholingana kwenye kuhitim na uzoefu. Kwa mfano, kwenye mnyororo wa thamani wa parachichi wanaume wanajihuisha zaidi na upandaji, upulizaji dawa na uvunaji, wakati wanawake hujihuisha zaidi na utunzaji vitalu, kuchambua/kupanga daraja na uuza sokoni.

Changamoto Muhimu

Uwekezaji zaidi umeonekana katika kilimo cha parachichi kwenye idadi ya miti iliopandwa, idadi ya nyumba za kufungashia ambazo zimeshajengwa na viwanda nya parachichi vinavyoendelea kujengwa. Hata hivyo, hizu ni changamoto na fursa ziliopo kwenye mnyororo wa thamani.

OPPORTUNITY	CHALLENGES
Kuongezeka kwa uzalishaji wa miche	Uhaba wa upatikanaji wa miche iliyothibitishwa ubora, uhaba wa maafisa ugani wanaotosha kwenye Kilimo cha mbogamboga na matunda, uhaba wa ujuzi wa kitaalam, na uelewa mbinu bora za kilimo mionganoni mwa wakulima, begu bora za mpunga, athari za kushambuliwa na wadudu na magonjwa
Kuongezeka uwekezaji kwenye miundombinu na vifaa husika	Uhaba wa maghala yenye vifaa muhimu nya kufungashia na vyumba baridi na upungufu wa huduma za usafirishaji na usafirishaji bandarini
Kuongezeka kwa Ubora na Viwango	Tija ndogo kwenye uzalishaji, kutokuwa na kiwango cha parachichi kitaifa na uelewa mdogo namna ya kushughulikia uhifadhi baada ya mavunog
Kuongezeka kwa upatikanaji wa soko	Sio Wakulima wote wamethibitishwa kidunia kutumia mbinu za kisasa za kilimo, Upungufu wa vifungashio, Ukosefu wa chama cha wauzaji parachichi nje ya nchi wanaoshughulikia masuala ya soko la ndani, na tofauti ya viwango nya cess kwa kila wilaya za mkoa mmoja
Fedha na Bima	Upatikanaji mdogo wa huduma za kifedha, ukosefu wa bima ya mazao na uelewa mdogo wa masuala ya kifedha na ujuzi wa ujasiriamali
Sera na mazingira wezeshaji	Usimamizi usioratibiwa wa sekta unasababisha kuyumba kwa soko

Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kupitia:

SAGCOT Centre Limited

Gholofa ya 5, Jengo la Ikon
Barabara ya Bains, Masaki
S.L.P 80945
Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 260 1024

+255 22 260 0146

Faxi: +255 22 260 2368

Barua Pepe: info@sagcot.co.tz

Tovuti: www.sagcot.co.tz